TOLEO LA NNE

April - Juni, 2023

# JARIDA LA MAMLAKA YA SERIKALI MTANDAO

## TANZANIA YANG'ARA MATUMIZI YA TEHAMA



- Ni Ripoti ya Benki ya Dunia *(GovTech Maturity Index)*
- Yapanda mpaka nafasi ya pili Afrika
- Nafasi ya kwanza Afrika Mashariki



Mhandisi Benedict B Ndomba

## KUTOKA KWA MKURUGENZI MKUU

Karibu katika toleo la nne la Jarida la Mtandaoni kutoka Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA). Katika jarida hili utasoma na kujifunza kuhusiana na kazi na huduma mbalimbali zinazofanywa na Mamlaka kama vile ujenzi wa mifumo inayoendana na mahitaji halisi ya Taasisi husika, utoaji wa huduma za ushauri na msaada wa kiufundi, uboreshaji wa njia za utoaji wa huduma za serikali mtandao, utengenezaji na uendeshaji wa mifumo na miundombinu ya TEHAMA Serikalini inayosaidia kuboresha ufanisi wa uendeshaji shughuli za utoaji wa huduma kwa Umma.

Hali kadhalika, katika Jarida hili utaweza kufahamu juhudi na shughuli mbalimbali zinazofanywa na Mamlaka katika utekelezaji wa dhana ya Serikali Mtandao.

Toleo hili ni muendelezo wa matoleo mengine yanayofuata yatakayokuhabarisha jitahada za e-GA katika kukuza na kuchochea matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) nchini, kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma za umma na kuleta mabadiliko ya kijamii na kiuchumi.

Nichukue fursa hii kukukaribisha tena katika kurasa hizi ili upate kuifahamu vizuri e-GA na shughuli mbalimbali inazozitekeleza.

*Nakutakia usomaji mwema*

# Yaliyomo

Kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu....i

Tanzania yang'ara Duniani matumizi ya TEHAMA Serikalini....1

Simbachawene aipongeza e-Ga Usimamizi wa TEHAMA Serikalini....3

Mtumishi Mahiri e-GA 2023: Mwaasha Semboko....4

Wakaguzi wa ndani watakiwa kutoa Ushauri wenye tija kwa Serikali katika Miradi na Mifumo Ya TEHAMA....5

ONGEZENI UBUNIFU: Naibu waziri UTUMISHI aielekeza e-GA....6

Mradi wa Digital Tanzania kuimarisha huduma za Kidijitali Nchini....7

Mfumo wa e-Board warahisisha shughuli za uaandaaji wa vikao....8

Katibu Mkuu UTUMISHI awahimiza Watumishi Wa e-GA Kuwa waadilifu....9

Kamati ya Ufundi Ya Serikali Mtandao yafanya Kikao cha kwanza Jijini Dodma....10

e-Ga Kuimarisha Mahusiano na Chuo Kikuu cha Mzumbe....12

Naibu Waziri Uwekezaji, Viwanda na Biashara anena faida za Mfumo wa MUVU....13

RC Dodoma aipongeza e-GA kwa Ubunifu wa Mifumo ya TEHAMA....14

Taasisi Za Umma Zahimizwa kuendesha vikao kwa njia ya Mtandao kupunguza Gharama....15

Ujazaji na Utengenezaji wa Dodoso sasa ni Kidijitali....16

OXYGEN : Programu ya Kijamii ya Mawasiliano iliyotengenezwa na Vijana wa Kitanzania....17

Makabidhiano ya ripoti ya CAG kwa Bodi ya wakurugenzi ya e-GA....18

# TANZANIA YANG'ARA DUNIANI MATUMIZI YA TEHAMA SERIKALINI.

1




Tanzania imetajwa kuwa miongoni mwa nchi zinazopiga hatua kubwa katika matumizi ya TEHAMA kwa kushika nafasi ya 26 kidunia na ya pili barani Afrika baada ya Mauritius.

Hayo yamebainishwa kwenye utafiti uliofanywa na Benki ya Dunia (WB) kuhusu ukomavu wa matumizi ya Teknolojia duniani katika utoaji wa huduma za serikali na ushirikishwaji wa wananchi (GovTech Maturity Index)

Ripoti hiyo ambayo inatokana na utafiti uliofanyika mwaka 2022 katika nchi 198 duniani, inabainisha kuwa Tanzania imefanikiwa kupanda daraja kutoka kundi B hadi kundi A na kushika nafasi ya 26 ikilinganishwa na mwaka 2021 ambapo ilishika nafasi ya 90.

Kwa upande wa Afrika, utafiti huo ulihusisha nchi 49 ikiwemo Tanzania na matokeo yamebaini kuwa, matumizi ya TEHAMA nchini yamepanda na kufikia asilimia 0.86 wakati Mauritius ina asilimia 0.864. Tanzania imepanda kutoka nafasi ya tano mwaka 2021 ambapo ilikuwa nyuma ya Afrika Kusini, Ghana, Kenya and Rwanda hadi nafasi ya pili mwaka 2022.

Katika ukanda wa Afrika Mashariki, **Tanzania imekuwa kinara kati ya nchi 13 zilizofanyiwa utafiti ambazo ni Burundi, Comoros, Djibouti, Somalia, Ethiopia, Sudan Kusini, Sudan, Eritrea, Kenya, Uganda, Rwanda, Seychelles na Tanzania ambapo matokeo yanaonyesha kuwa Tanzania imepanda kutoka nafasi ya tatu mwaka 2021 hadi nafasi ya kwanza mwaka 2022.**

Kwa mujibu wa ripoti hiyo iliyotolewa mwezi Machi mwaka huu, sekta za elimu, afya, fedha na kilimo nchini Tanzania ni sekta zinazoongoza katika utoaji wa huduma za serikali kupitia TEHAMA na kurahisisha upatikanaji wa huduma hizo kwa wananchi.

Aidha, ripoti hiyo imebainisha kuwa, mafanikio hayo yanatokana na utayari wa serikali wa kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika Taasisi za Umma, uwepo wa dira mahususi kuhusu sera ya TEHAMA, Sheria, viwango na miongozo ya Serikali Mtandao, mikakati madhubuti na utekelezaji wake unaosimamiwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA).

Utafiti huo uliangalia maeneo manne ambayo ni mipango na usimamizi wa TEHAMA serikalini ikiwa ni pamoja na uwepo wa Miundombinu ya Kuhitafadhia Mifumo (Data Centers), Miongozo ya kubadilishana taarifa kwa mifumo ya Serikali na uwepo wa mifumo shirikishi, ushirikishwaji wa wananchi kupitia majukwaa ya kidijitali kwa kupima utaratibu unaotumika kwa wananchi kutoa maoni kwa njia ya kidijitali, majukwaa ya kidijitali yanayotumika kushirikisha wananchi, taarifa za wazi pamoja na tovuti za Serikali.

Eneo la mwisho lililoangaliwa ni uwepo wa nyenzo wezeshi za teknolojia serikalini kwa kuangalia Sera ya ubunifu wa teknlojia, sheria na kanuni, ujuzi katika masuala ya dijitali na programu mbalimbali zinazotumika kuimarisha TEHAMA serikalini.

Aidha, utafiti huo umetaja mifumo ambayo imesaidia kuimarika kwa matumizi ya TEHAMA katika Taasisi za Umma nchini kuwa ni pamoja na mfumo wa e-Mrejesho ambao unawawezesha wananchi kuwasiliana moja kwa moja na Taasisi za umma kwa njia ya kidijitali, ili kuwasilisha maoni, mapendekezo, maswali, pongezi au malalamiko yao sambamba na kufuatilia utekelezaji wake ndani ya Taasisi husika.

Mifumo shirikishi katika Taasisi za Umma Vituo vya kuhifadhia Mifumo (Government Data Centers), Mifumo hiyo ni pamoja na Mtandao wa Mawasiliano Serikalini ambao umeziunganisha Wizara, Idara na Wakala 72 pamoja na Halmashauri 77, Kituo cha kuhifadhia

data cha serikali, Mfumo wa ofisi Mtandao ambao huwezesha na kurahisisha shughuli za utawala za kila siku ndani ya Taasisi za umma ikiwa ni pamoja na mzunguko wa nyaraka ndani ya Taasisi.

Mifumo mingine ni huduma za mtandao ambazo hurahisisha upatikanaji wa huduma mbalimbali kwa wananchi kidijitali, huduma hizo ni pamoja na Ajira portal, Mfumo wa Malipo Serikalini (GePG), Maombi na utoaji wa leseni, hati ya kusafiria n.k.

Vilevile, Mfumo wa MGOV ambao ni mfumo jumuishi wa utoaji wa huduma kwa njia ya simu za mkononi Serikalini, mfumo huu unarahisisha na kuharakisha utoaji wa huduma. Mfumo wa mGOV umeunganishwa na watoa huduma wote wa simu za mikononi nchini Tanzania na unatoa huduma za ujumbe mfupi wa maandishi (SMS) kupitia namba jumuishi 15200 na 15201 pamoja na huduma za menyu ya USSD kupitia namba jumuishi *152*00#.


Aidha, mfumo wa MGOV unaruhusu Taasisi za Umma kutoa huduma kupitia namba binafsi za Taasisi, mfano wa namba binafsi za ***Taasisi ni199 ya Wizara ya Afya inayotoa huduma na taarifa za COVID-19, na *113# ya PCCB inayotoa huduma ya kuripoti matukio ya rushwa. Hadi kufikia Julai, 2022 Taasisi zaidi ya 254 zinatumia mfumo wa mGOV kutoa huduma, baadhi ya huduma hizo ni SMS za manunuzi ya umeme (LUKU), SMS za huduma za malipo ya Serikali (GePG), Huduma za kikodi (TRA), Huduma za Ardhi, Huduma za afya (NHIF, CHF) nk.***

Pia, Mfumo wa GoVESB ambao ni Mfumo shirikishi unaounganisha mifumo ya Taasisi za Umma kuwasiliana na kubadilishana taarifa, Mfumo huu unatumika kupunguza urudufu wa mifumo pamoja na kurahisishsa utendaji kazi wa taasisi za umma na utoaji wa huduma kwa wananchi.

Mingine ni ***Mfumo wa ukusanyaji wa malipo Serikalini (GePG), Mfumo wa 'Ajira Portal' ambao hurahisisha utoaji wa matangazo na maombi ya nafasi za kazi kwa njia ya kidijitali. Mfumo wa Ulipaji Serikalini (MUSE), Mfumo wa taarifa za Usimamizi wa Ushuru na forodha (TANCIS), Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Watumishi Serikalini (HCMIS), Mfumo wa manunuzi mtandaoni (TANePS) na Tovuti Kuu ya Serikali.***

Licha ya kuimarika kwa matumizi ya TEHAMA nchini, ripoti hiyo imebainisha kuwa pengo la kidijitali limeongezeka katika nchi masikini zenye uchumi wa chini na wa kati kutokana na uhaba wa fedha pamoja na kutokuwepo kwa sera madhubuti kuhusu TEHAMA. Utafiti huu umekuwa na manufaa kwa mataifa mbalimbali kwakuwa unaangalia zana zinazotumika katika kuimarisha TEHAMA kwenye mataifa mbalimbali pamoja na kuainisha maeneo yanayotakiwa kuboreshwa zaidi.





ega_tanzania

# 2 WAZIRI SIMBACHAWENE AIPONGEZA e-GA USIMAMIZI WA TEHAMA SERIKALINI



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. George Simbachawene, ameipongeza Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) kwa jitihada kubwa inazozifanya katika kukuza na kuimarisha Serikali Mtandao nchini.

Mhe. Simbachawene alitoa pongezi hizo Juni 13 mwaka huu alipofanya ziara ya kikazi katika Ofisi za Mamlaka ya Serikali Mtandao zilizopo Mji wa Serikali Mtumba jijini Dodoma, kwa lengo la kukagua utekelezaji wa majukumu ya e-GA katika usimamizi wa matumizi ya TEHAMA kwenye taasisi za umma.

Alisema kuwa, kuimarika kwa matumizi ya TEHAMA katika taasisi za umma, kunatokana na usimamizi mzuri wa e-GA katika kuimarisha jitihada za serikali mtandao, hali ambayo imesaidia kuongezeka kwa ufanisi wa utendaji kazi wa shughuli za serikali pamoja na utoaji huduma kwa wananchi.

*"Bila Serikali Mtandao mambo mengi yangekuwa hayaendi sawa, e-GA mmetumia teknolojia kurahisisha na kufanikisha shughuli nyingi za Serikali kufanyika kwa wakati pamoja na kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi, nawapongeza sana", alisema.*

Pamoja na pongezi hizo, pia Waziri aliitaka e-GA kuimarisha Kituo cha Utafiti, Ubunifu na Uendelezaji wa Serikali Mtandao (eGovRIDC) ili kutengeneza vijana wengi zaidi ambao watabuni mifumo inayotatua changamoto zilizopo.

"Ni muhimu kuimarisha kituo cha utafiti na ubunifu ili kuandaa na kutengeza vijana mahiri katika masuala ya teknolojia kwa maslahi mapana ya taifa, na sisi upande wa Wizara tutahakikisha tunatoa msaada wa kutosha pale mtakapohitaji", alisema.

Aidha, aliitaka e-GA kuendelea kuwajengea uwezo watumishi wake kwa kuhakikisha wanapata mafunzo ya muda mfupi na mrefu kutoka ndani na nje ya nchi, ili kuwaongeza ujuzi wa kukabiliana na mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia katika usanifu wa mifumo, miundombinu pamoja na miradi ya TEHAMA yenye tija kwa taifa.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu e-GA Eng. Benedict Ndomba, alimshukuru Waziri kwa kufanya ziara hiyo pamoja na ushirikiano mkubwa anaoupata kutoka Wizarani katika utekelezaji wa majukumu ya taasisi.



Aidha alisema kuwa, e-GA itaendelea kuimarisha kituo cha utafiti na ubunifu pamoja na kutoa elimu kwa Taasisi za Umma katika usimamizi na uzingatiaji wa Sheria, kanuni, viwango na miongozo ya Serikali Mtandao ili kuhakikisha mifumo na miradi yote ya TEHAMA katika taasisi za umma inakuwa na tija kwa taifa.

# Mtumishi Mahiri e-GA 2023: MWANAASHA SEMBOKO

3

*Na Mwandishi wetu*
*23 mei, 2023*




Afisa TEHAMA Mkuu kutoka Idara ya Usimamizi wa Huduma za TEHAMA Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) ***Bi. Mwanaasha Semboko*** ameibuka mshindi katika kinyang'anyiro cha kumchagua Mtumishi Mahiri wa Mamlaka kwa mwaka 2023.

Hayo yalibainishwa na Meneja wa Rasilimali Watu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao Bw. Erick Kalembo wakati wa mahojiano na mwandishi wetu jijini Dar Es Salaam kwenye kilele cha maadhimisho ya siku ya Wafanyakazi Duniani (Mei Mosi) 2023.

"Mchakato huu wa kupata mtumishi mahiri ulianza kwa kufanya uchaguzi wa mfanyakazi bora ndani ya idara pamoja na vitengo, ambao ulikua wa wazi na huru kwa watumishi wenyewe kufanya tathmini kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa na kisha kupiga kura", alisema Bw. Kalembo.

Baada ya kupata mtumishi bora kwenye kila idara na vitengo Menejimenti ya Mamlaka ilifanya kikao na kupokea orodha ya majina ya watumishi waliochaguliwa na kisha kupiga kura kwa ajili ya kuwapata watumishi watatu bora wa Mamlaka, ambapo Bi. Mwanaasha aliibuka mshindi baada ya kupata kura nyingi akifuatiwa na **Bw. Masuka Manyasi** na **Bi. Dhulfa Abdallah** aliyeshika nafasi ya tatu.

Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyakazi (TUGHE) kutoka e-GA ***Bw. Asraji Juma,*** alisema mojawapo la takwa la kisheria kwenye Chama cha Wafanyakazi ni lazima kila taasisi ichague watumishi bora katika idara na vitengo ambao kati yao atapatikana mtumishi mahiri wa taasisi baada ya watumishi hao kushindanishwa, na kuipongeza e-GA kwa kuzingatia sheria hiyo.

Naye Bi. Mwanaasha aliishukuru Menejimenti ya e-GA kwa kumchagua kwakuwa inaonesha kuthamini mchango na juhudi zake katika taasisi jambo linalompa moyo kuendelea kufanya kazi vizuri zaidi kwa kuzingatia sheria na taratibu za utumishi wa umma.

***"Ninaishukuru sana Manejimenti ya e-GA kwa kuniona, kuniamini na kunichagua kuwa Mtumishi Mahiri kwa mwaka 2023, nimefarijika sana kwani sikutegemea na sikujua kama watu wanaona kazi kubwa ninayoifanya na kuithamini pia ninaahidi sitowaangusha nitafanya kazi kwa moyo wa kujituma, bidii na weledi mkubwa zaidi", alisema Bi. Mwanaasha.***

Vilevile, Mwanaasha aliwashukuru watumishi wote wa Mamlaka hususan timu yake ya kukusanya madeni, kwa kukubali mawazo na ushauri mbalimbali aliokua akiutoa pamoja na ushirikiano wao katika kutimiza majukumu yao ya kila siku jambo liliyopelekea yeye kuibuka kuwa mtumishi mahiri.

Pia, amewashauri watumishi wote kufanya kazi kwa kujituma, kujitoa na kujiamini na kukumbuka kuwa sikuzote hakuna kazi ngumu, kitu cha muhimu ni kila mtumishi kupambana na kuhakikisha anatatua changamoto zilizopo ili kufikia malengo ya taasisi.

Bi. Mwanaasha pamoja na watumishi wote waliochaguliwa kuwa wafanyakazi bora mwaka 2023 walipewa zawadi za fedha tasilimu ikiwa ni motisha kwa watumishi wengine kuendelea kufanya kazi vizuri zaidi na kwa weledi.

# WAKAGUZI WA NDANI WATAKIWA KUTOA USHAURI WENYE TIJA KWA SERIKALI KATIKA MIRADI NA MIFUMO YA TEHAMA

4



Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali Bw. Paison Mwamnyasi, amewataka Wakaguzi wa Ndani kuzingatia sheria, kanuni, viwango na miongozo ya Serikali Mtandao wanapofanya ukaguzi kwenye miradi na Mifumo ya TEHAMA, ili waweze kutoa ushauri wenye tija kwa serikali kupitia taarifa zao za ukaguzi.

Bw. Mwamnyasi aliyasema hayo Juni 05, Mwaka huu wakati wa ufunguzi wa awamu ya pili ya mafunzo maalum kwa Wakaguzi wa Ndani kutoka halmashauri na Tawala za Mikoa 13 za Tanzania Bara.

Alisema kuwa, mafunzo ya ukaguzi wa mifumo na miradi ya TEHAMA Serikalini ni muhimu kwa Wakaguzi wa Ndani kwa kuwa yanawajengea uwezo katika utendaji kazi na kurahisisha shughuli za ukaguzi sambamba na kutoa ushauri wenye tija kwa serikali.

***"Ukielewa namna mifumo inavyofanya kazi, unaweza kukagua ipasavyo, na tutaepuka kutaja majina ya watu katika taarifa zetu za ukaguzi badala ya mifumo, sisi Wakaguzi tunatambua kuwa miongozo ya ukaguzi inaeleza kutokagua sehemu ambayo hauna uelewa nayo kwa kuwa unaweza kutoa maoni na ushauri kwa Serikali ambao hauna tija" aliongeza.***

Aidha, Mkurugenzi wa Udhibiti na Usalama wa TEHAMA Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Bw. Sylvani Shayo, aliwasisitiza Wakaguzi wa Ndani kutumia Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao wakati wa kusimamia na kufanya ukaguzi wa miradi na mifumo ya TEHAMA katika taasisi zao.

Alibainisha kuwa, e-GA kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wanaendelea na jitihada za kutoa mafunzo kwa Wakaguzi wa Ndani ili waweze kufanya ukaguzi katika eneo la TEHAMA kwa ufanisi.

"Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao ni nyenzo muhimu katika ukaguzi wa miradi na mifumo ya TEHAMA katika taasisi za umma, na ikiwa wakaguzi wa ndani mtazingatia vema miongozo na sheria hizo mtafanya ukaguzi wenye tija na maslahi kwa taifa", alisema Bw. Shayo.

Naye Meneja wa Udhibiti wa Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao Bi. Sultana Seiff alisema, e-GA haitaki kuacha kada yoyote nyuma katika matumizi ya TEHAMA kwakuwa dunia ya sasa inaendeshwa kidijitali, hivyo wakaguzi wa ndani wanapewa mafunzo hayo ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi na kuboresha utoaji wa huduma za Serikali kwa njia ya kidijitali.

Mafunzo hayo ya siku tano yalifanyika mkoani Morogoro kuanzia Juni 05 hadi 09 mwaka huu,- na kuhusisha wakaguzi wa ndani 110 kutoka Halmashauri na Tawala za Mikoa ya Dodoma, Tabora, Singida, Kigoma, Mara, Dar es Salaam, Morogoro, Shinyanga, Rukwa, Kagera, Geita, Simiyu na Katavi. Awamu ya kwanza ya mafunzo hayo yalifanyika Machi mwaka huu ambapo jumla ya Wakaguzi wa Ndani 133 kutoka Halmashauri na Tawala za Mikoa 13 za Tanzania Bara, walishiriki.

# ONGEZENI UBUNIFU: NAIBU WAZIRI UTUMISHI AIELEKEZA e-GA

5



Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Ridhiwani Kikwete, amewata watumishi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) kufanya kazi kwa bidii na kuongeza ubunifu katika eneo la TEHAMA, ili kuibua mifumo itakayoweza kutatua matatizo ya watanzania.

Ridhiwani alisema hayo Juni 13, Mwaka huu wakati wa kikao kazi cha watumishi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao kilichofanyika katika ofisi za Mamlaka zilizopo Mji wa Serikali Mtumba jijini Dodoma.

Kwakuwa dunia inaendeshwa kidijitali, matumizi ya teknolojia hatuwezi kuyakwepa hivyo, watumishi wa Mamlaka hamna budi kuongeza ubunifu katika eneo la TEHAMA kwa kutengeneza mifumo inayotatua matatizo tuliyonayo, alisema.

“Tunategemea kupitia e-GA mambo yote yataenda kidijitali, mmefanya kazi kubwa sana tunaiona kwakuwa huduma nyingi za serikali kwa sasa zinapatika kidijitali lakini ni lazima muendeleze ubunifu kwakuhakikisha mnaibua mifumo mbalimbali inayotatua matatizo tuliyonayo”, alisisitiza.

Aliongeza kuwa, teknolojia hukua na kubadilika kila siku, hivyo ni lazima watumishi wa e-GA wakajiendeleza kwa kupata mafunzo ya mara kwa mara ya muda mfupi na mrefu, ndani na nje ya nchi ili kuendana na mabadiliko hayo.

“Wizara ipo tayari muda wowote kutoa msaada pindi mtakapohitaji, ni lazima mjifunze kutoka kwa wenzetu waliotuzidi kwa upande wa teknolojia, hivyo uongozi wa e-GA muweke utaratibu wa kuwawezesha watumishi wenu kupata mafunzo ndani na nje ya nchi”, alisema.


Naye Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Eng. Benedict Ndomba, aliahidi kutekeleza maagizo ya Naibu Waziri ikiwa ni pamoja na kuandaa utaratibu wa kuwajengea uwezo watumishi wake kwa kupata mafunzo mbalimbali ili kuendana na mabadiliko ya teknolojia.

Kikao kazi hicho kiliongozwa na Mhe. George Simbachawene Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Naibu Waziri Mhe. Ridhiwani Kikwete pamoja na Katibu Mkuu Bw. Juma Mkomi.



# MRADI WA *DIGITAL TANZANIA* KUIMARISHA HUDUMA ZA KIDIJITALI NCHINI

6



Mradi wa 'Digital Tanzania' unatarajiwa kuimarisha utoaji wa huduma kwa njia ya kidijitali kati ya Serikali, Wananchi pamoja na Wafanyabiashara sambamba na kuchochea uwekezaji katika miradi ya kidijitali nchini.

Hayo yamebainishwa na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Eng. Benedict Ndomba Mei 23, mwaka huu alipozungumza na mwandishi wetu kuhusu mradi huo ofisini kwake jijini Dodoma.

Alibainisha kuwa, mradi huo una malengo makuu mawili ambayo ni kuongeza upatikanaji wa huduma za mtandao wa intaneti zenye gharama nafuu na ubora wa juu kwa serikali, wafanyabiashara na wananchi sambamba na kuboresha uwezo wa serikali wa kutoa huduma za umma kidijitali.




Mwakilishi wa Benki ya Dunia anayesimamia mradi wa Digital Tanzania Bi.Isabel Neto akizungumza wakati wa kikao.

"Lengo la pili la mradi huo ni kuchangia upatikanaji wa intaneti na upatikanaji wa huduma za umma kidijitali ili kuwezesha sekta binafsi kuwekeza katika miradi ya kidijitali na kuongeza ajira", alisema Ndomba.


Kupitia mradi huo e-GA inayo majukumu matatu ambayo ni upanuzi wa mtandao wa serikali, uboreshaji wa vituo vya kuhifadhia data pamoja na masafa ya intaneti 'bandwith', ambapo kupitia mradi huo jumla ya vituo 660 vinatarajia kunufaika.

Mei 23, mwaka huu Wawakilishi wa Benki ya Dunia wanaosimamia mradi huo pamoja na wajumbe wa kamati hiyo walikutana ofisi za e-GA Mtumba jijini Dodoma na kufanya kikao cha majadiliano juu ya mradi huo ambao utekelezaji wake unaendelea.

Mradi wa 'Digital Tanzania' unaofadhiliwa na benki ya Dunia unatekelezwa kwa usimamizi wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari pamoja na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kushirikiana na Taasisi mbalimbali zinazohusika na TEHAMA ikiwemo e-GA.




Wawakilishi wa Benki ya Dunia wanaosimamia mradi wa Digital Tanzania kutoka kushoto ni Raymond Mbishi, Sara Ballan, Isabella Neto na Paul Seaden wakiwa katika picha ya pamoja na Mkurugenzi Mkuu e-GA Eng. Benedict Ndomba katikati (Mstari wa kwanza) pamoja na wajumbe wengine wa mradi huo mara baada ya kumaliza kikao katika Ofisi za e-GA Dodoma



# MFUMO WA e-BOARD WARAHISISHA SHUGHULI ZA UAANDAAJI WA VIKAO

7




Mfumo wa e-board umerahisisha na kuwezesha uratibu wa shughuli zote za uandaaji wa vikao mbalimbali vya bodi na menejimenti katika Halmashauri na Taasisi za Umma.

Mfumo huo wa kidigitali unawezesha sekretarieti kuandaa yatokanayo kwenye kikao, wajumbe kupiga kura na kuwawezesha wajumbe wa menejimenti kutengeneza ripoti za utendaji kazi katika vipindi mbalimbali vya mwaka.

Meneja wa Kituo cha Utafiti na Ubunifu na Uendelezaji wa Serikali Mtandao (eGovRIDC) Mamlaka ya Serikali Mtandao Dkt.Eng Jaha Mvulla alisema kuwa, mfumo wa e- board umebeba taswira ya shughuli zote zinazofanyika katika utaratibu wa kawaida wa uandaaji vikao kwa lengo la kuboresha uratibuji wa vikao vya bodi, menejimenti na halmashauri.

“Mfumo unalenga kuwasaidia wahusika wa kuandaa vikao yani sekretarieti katika kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi pamoja na kuwaongozea ufanisi wajumbe katika utekelezaji wa majukumu yao kupitia TEHAMA” Alifafanua.

Jaha alibainisha kuwa, mfumo wa e-board umetengenezwa na kusanifiwa na wataalamu wa ndani kutoka e-GA na umekidhi uhitaji wa mchakato mzima wa uaandaji wa vikao kuanzia kwenye utengenezaji wa ajenda, utumaji wa notisi kwa wajumbe, utengenezaji wa makalablasha ya vikao, uchukuaji wa yatokanoyo, hadidu za rejea, upigaji kura pamoja na ripoti mbalimbali za utekelezaji.

Aliongezea kuwa, e-GA iliazimia kutengeneza mfumo wa e-Board ili kusaidia taasisi za umma kuwa na ufanisi kwenye eneo la kuratibu vikao baada ya kuona uhitaji mkubwa wa matumizi ya TEHAMA kwenye eneo hilo.

> ***“Hadi hivi sasa, takribani taasisi 18 zimekwishajiunga na Mfumo wa e-Board na tunandelea kupokea na kuzifanyia kazi barua za maombi ya kuunganishwa kwenye Mfumo huu kutoka Taasisi mbalimbali za Umma lakini pia nitoe wito kwa taasisi nyingine kutumia mfumo huu ili kuongeza ufanisi katika uendeshaji wa vikao”***, alisisitiza Jaha.


ega_tanzania

# KATIBU MKUU UTUMISHI AWAHIMIZA WATUMISHI WA e-GA KUWA WAADILIFU

8

Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Bw. Juma Mkomi, amewataka watumishi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) kuzingatia maadili ya utumishi wa umma ili kulinda maslahi ya taifa.

Mkomi alitoa kauli hiyo Juni 13, Mwaka huu wakati wa kikao kazi cha watumishi wa e-GA na viongozi wa Wizara, kilicholenga kujadili utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka.

Alisema kuwa, watumishi wa e-GA wanashiriki katika kazi muhimu zinazohusu mifumo na miundombinu muhimu ya TEHAMA serikalini hivyo, wanapaswa kuwa waadilifu kwa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi, pamoja na kutunza siri ili kulinda maslahi ya nchi.

"Nyinyi ndio mnahusika na mifumo ya serikali ikiwemo mifumo nyeti inayohusu rasilimali na usalama wa taifa, hakikisheni nafasi mliyonayo mnaitumia kutekeleza majukumu yenu tu kwa uadilifu na kutunza siri ili kulinda taifa letu", alisema.

Vilevile aliwapongeza watumishi hao kwa weledi na utendaji kazi mzuri katika utekelezaji wa majukumu yao, hali ambayo inachangia ukuaji wa Serikali Mtandao katika taasisi za umma.

"Napokea simu nyingi sana aidha kutoka kwa Makatibu Wakuu au Wakuu wa taasisi za umma, wakiomba vijana kutoka e-GA hii inaonesha ni jinsi gani mlivyo wazuri katika utendaji kazi wenu" alisisitiza.

Ili kuongeza ufanisi na ubunifu katika TEHAMA, Mkomi aliutaka uongozi wa Mamlaka kuwajengea uwezo watumishi wake kwa kuwapa mafunzo ya muda mrefu na mfupi ndani na nje ya nchi.

Alisema, teknolojia hukua na kubadilika kila mara, hivyo ni vema Mamlaka ikaweka utaratibu wa kuwajengea uwezo watumishi wake ili kuweza kukabiliana na mabadiliko hayo.




Kikao kazi hicho kilifanyika katika Ofisi za e-GA zilizopo Mji wa Serikali Mtumba, jijini Dodoma, na kuongozwa na Mhe. George Simbachawene Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Naibu Waziri Mhe. Ridhiwani Kikwete pamoja na Katibu Mkuu Bw. Juma Mkomi.



# KAMATI YA UFUNDI YA *SERIKALI MTANDAO* YAFANYA KIKAO CHA KWANZA JIJINI DODOMA

9



Kamati ya ufundi ya serikali mtandao imefanya kikao cha kwanza na kujadili mambo mbalimbali ikiwa ni pamoja na namna ya utekelezaji wa majukumu yake, ili kuhakikisha jitihada za serikali mtandao zinaimarika na kuleta tija kwa Umma.

Kikao hicho kilifanyika Juni 23, Mwaka huu katika Ofisi za Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) jijini Dodoma, na kuongozwa na Kaimu Mwenyekiti Bw. Eric Kitali Mkurugenzi wa TEHAMA, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Akizungumza katika kikao hicho, Bw. Eric alisema kamati hiyo ipo kwa mujibu wa kifungu Na. 17 cha sheria ya Serikali Mtandao ya mwaka 2019, ambapo miongoni mwa majukumu yake ni kutoa ushauri wa kitaalamu, ili kuhakikisha utekelezaji wa Serikali Mtandao unakuwa wenye tija na kuongeza ufanisi katika utendaji kazi na utoaji wa huduma kwa umma.

Alisema kuwa, kamati hiyo ina wajumbe wachache ikilinganishwa na idadi ya Wizara na Taasisi za serikali zilizopo, na kuwasihi wajumbe wote kutenda haki kwa kuwajibika na kuhakikisha wanatoa ushauri wenye tija katika eneo la TEHAMA ili kuhakikisha serikali mtandao inaimarika na kuleta tija kwa Serikali

"Ikiwa kamati hii itafanikiwa kuifanya mifumo ya TEHAMA katika taasisi za umma izungumze tutakuwa tumeisaidia sana serikali, kwani itaokoa rasilimali fedha pamoja na rasilimali watu", alisisitiza.

Akiyataja baadhi ya majukumu ya kamati hiyo kwa mujibu wa kifungu Na 17 (4) cha Sheria ya Serikali Mtandao ya mwaka 2019, Katibu wa Kamati hiyo Bw. Sylvani Shayo ambaye pia ni Mkurugenzi wa Udhibiti na Usalama wa TEHAMA e-GA alisema ni pamoja na;

Kupitia na kutoa mapendekezo juu ya Sera ya Serikali Mtandao itakayotekelezwa katika taasisi za umma, kupitia na kutoa mapendekezo juu mpango mkuu wa Serikali mtandao na mkakati wake utakaotekelezwa na taasisi zote za umma, kupitia na kutoa mapendekezo juu ya miradi na program za kitaifa za serikali mtandao, na kutoa miongozo ya kiufundi katika kutatua migogoro kwenye utekelezaji wa miradi mikubwa ya TEHAMA katika taasisi za umma.



Majukumu mengine ni kuishauri kamati ya kitaifa ya serikali mtandao kuhusu masuala ya serikali mtandao, kuandaa ripoti za robo mwaka na kuziwasilisha katika kamati hiyo, pamoja na kutekeleza majukumu mbalimbali yatakayotolewa na Mamlaka ya Serikali Mtandao na kamati ya kitaifa ya Serikali Mtandao.

Wizara ya Maji, Mamlaka ya Serikali Mtandao (wajumbe 02), Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), The Nelson Mandela African Institution of Science and Technology (NM-AIST), Benki Kuu ya Tanzania (BOT), Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), Wakala wa Ufilisi na udhamini (RITA), Idara ya Uhamiaji, Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, na Wizara ya Kilimo.




Aidha, kamati hiyo iliazimia kuweka mikakati ya kupunguza urudufu wa mifumo na kuhakikisha mifumo yote ya TEHAMA, katika taasisi za umma inawasiliana na kubadilishana taarifa kupitia Mfumo Mkuu wa ubadilishanaji taarifa serikalini (GoVESB).

Katika hatua nyingine, kamati ilimchagua Bi. Connie Francis Mkurugenzi wa TEHAMA Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), kuwa Makamu Mwenyekiti wa kamati hiyo.

Wajumbe wa kamati hiyo ni Wakuu wa TEHAMA kutoka Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali wakiongozwa na Mwenyekiti Bw. Priscus Kiwango kutoka Ofisi ya Rais, Menejiment ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Katibu Bw. Sylvani Shayo ambaye ni Mkurugenzi wa Udhibiti na Usalama wa TEHAMA Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA).

Wajumbe wengine ni kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu-Sera, Uratibu na Bunge, Ofisi ya Rais- Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Afya, Wizara ya Ardhi, Nyumba na maendeleo ya makazi, Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa,

# e-GA KUIMARISHA MAHUSIANO NA CHUO KIKUU CHA MZUMBE

10



Mamlaka ya Serikali Mtanda (e-GA) inalenga kuimarisha zaidi uhusiano wake na Chuo Kikuu cha Mzumbe kupitia mkataba wa makubaliano (MOU) unaotarajiwa kufanyiwa maboresho hivi karibuni.

Hayo yameelezwa na Mkurugenzi Mkuu wa e-GA Eng. Benedict Ndomba, wakati wa kikao cha pamoja kati ya e-GA na Chuo Kikuu cha Mzumbe kilichofanyika Juni 14 mwaka huu katika ofisi za e-GA jijini Dodoma, kwa ajili ya kujadili utekelezaji wa mkataba wa kwanza wa makubaliano (MOU).

Ndomba alisema kuwa, Mkataba wa kwanza wa makubaliano ulisainiwa Novemba 13, 2020 na umekuwa na mchango mkubwa katika kuimarisha mahusiano kati ya taasisi hizi mbili katika kuimarisha jitihada za Serikali Mtandao.

Naye Mkurugenzi wa TEHAMA Chuo Kikuu cha Mzumbe Dkt. Mohamed Ghasia, amesema kuwa chuo hicho kimepata mafanikio makubwa kutokana na mkataba huo ikiwa ni pamoja na kupata mafunzo mbalimbali kuhusu Serikali Mtandao, Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao, uwekaji wa taarifa katika tovuti , mfumo wa ofisi mtandao (e-office), barua pepe za serikali (GMS) pamoja na mafunzo ya usalama wa mtandao.

Pamoja na mafanikio hayo, Dkt. Ghasia pia alitaja baadhi ya changamoto zilizopo ambazo zinatakiwa kufanyiwa kazi kupitia MOU mpya itakayoandaliwa hivi karibuni ili kutatua changamoto hizo.

***"Tunaona kuna pengo kubwa kati ya wahitimu wa vyuo vikuu na ujuzi unaohitajika katika soko la ajira, hivyo e-GA ikiwa ni mdau wetu mkubwa mtatusaidia sisi wa vyuo vikuu kufahamu maeneo tunayotakiwa kuboresha katika mitaala yetu ili kutengeneza vijana wanaoendana na soko la ajira",*** alisema Ghasia.

Aliongeza kuwa, ni vema mifumo ya serikali ikawa endelevu na hivyo baadhi ya mifumo hiyo ikaingizwa katika mitaala ya vyuo vikuu ili kuwasaidia wanafunzi kuifahamu na kuweza kuitumia wanapoajiriwa katika taasisi za umma.

Ni vizuri pia wataalamu wa e-GA kuweka utaratibu wa kutembelea Vyuo Vikuu ili kutoa mafunzo kwa wanafunzi kuhusu mabadiliko ya teknolojia yaliyopo pamoja na mahitaji katika soko la ajira ili kuwatia hamasa katika masomo yao, alisema Dkt. Ghasia.

Mkataba mpya wa makubaliano kati ya e-GA na Chuo Kikuu cha Mzumbe unatarajiwa kuimarisha tafiti na bunifu za TEHAMA, kuandaa mikutano na vikao vya pamoja kati ya e-GA na Vyuo Vikuu pamoja na kuandaa eneo lenye mazingira wezeshi kwa wanafunzi kujifunza kwa vitendo.


ega_tanzania

# NAIBU WAZIRI UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA ANENA FAIDA ZA MFUMO WA MUVU

11

Naibu Waziri Uwekezaji, Viwanda na Biashara Mhe.Exaud Kigahe, amesema Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (MUVU) utasaidia kutatua changamoto mbalimbali zilikokuwa zikivikabili vyama vya ushirika nchini.



Mhe. Kigae alitoa kauli hiyo Juni 13, Mwaka huu wakati wa uzinduzi wa wiki ya maadhimisho ya siku ya Ushirika Duniani, yaliyofanyika katika viwanja vya Nanenane Ipuli Mkoani Tabora.

Alisema, kumekuwa na changamoto mbalimbali katika uendeshaji wa vyama vya ushirika kwa muda mrefu ikiwemo wakulima kudhulimiwa mazao yao hali iliyopelekea baadhi ya wakulima kujiondoa katika vyama hivyo, lakini kupitia mfumo wa MUVU mkulima ataepukana na tatizo hilo.

''Hapo mwanzo kulikuwa na changamoto kubwa kwenye hivi vyama vya ushirika,mpaka ilifikia hatua wakulima wakakasirika na wengine kujiondoa kwenye vyama, sasa huu Mfumo umeleta maboresho makubwa yatakayosaidia mkulima kutokupunjwa mazao yake'', alisema.

Meneja wa TEHAMA Tume ya Maendeleo ya Vyama vya Ushirika (TCDC), Hermes Sotter alisema, Mfumo wa MUVU umeongeza uwazi katika uendeshaji wa vyama vya ushirika kwakuwa umeunganishwa na Mfumo wa Mizani ya Kidigitali unaomuwezesha Mkulima kupokea taarifa za mzigo wake ikiwemo risiti na ujumbe mfupi wa maandishi kupitia simu yake ya mkononi, mara baada ya kupimiwa kwenye chama cha ushirika.

Nao wakulima kutoka katika vyama mbalimbali vya Ushirika, wameeleza kuridhishwa na mfumo huo kwakuwa hivi sasa wanapata taarifa zote kuhusu mazao yao tofauti na ilivyokuwa hapo awali hivyo hawana wasiwasi tena kwani kila kitu kinapitia kwenye Mfumo.

Mfumo wa MUVU umetengenezwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) kwa kushirikiana na Tume ya Maendeleo ya Ushirika-TCDC kwa lengo la kutatua changamoto mbalimbali zilizokuwa zikiikabili sekta ya ushirika.

# RC DODOMA AIPONGEZA e-GA KWA UBU NIFU WA MIFUMO YA TEHAMA

12

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mhe. Rosemary Senyamule, ameipongeza Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) kwa bunifu mbalimbali za Mifumo ya TEHAMA inayorahisisha utendaji kazi na utoaji wa huduma kwa wananchi.

Rosemary alitoa pongezi hizo Aprili 25, Mwaka huu wakati alipotembelea banda la maonesho la e-GA katika maadhimisho ya wiki ya kitaifa ya ubunifu na MAKISATU, yaliyofanyika April 24 hadi 28 mwaka huu katika viwanja vya Jamhuri jijini Dodoma.

**"Taasisi yetu ya Mamlaka ya Serikali Mtandao kwa kweli mmekuwa mkifanya kazi nzuri, mmetutoa katika yale mambo ya kizamani ya kurundikana kwa makaratasi ofisini mmetuletea Mifumo ambayo sasahivi hata kama nisipokuwa ofisini bado naweza kujibu barua, mimi nawapongeza sana" alisema Rosemary.**

Katika Maonesho hayo, e-GA kupitia kituo chake cha Utafiti na Ubunifu wa Maendeleo ya Serikali Mtandao ***(eGovRIDC)*** imeonesha teknolojia na bunifu mbalimbali zilizobuniwa na vijana wa kitanzania ambazo zimelenga kuimarisha na kukuza jitihada za Serikali Mtandao.

Baadhi ya Mifumo iliyooneshwa ni pamoja na; Mfumo wa kuratibu shughuli za kimawasiliano kwa kupiga simu kwa Taasisi mbalimbali za Umma ***(Intergrated CallCenter System & CRM),*** Ubunifu unaotumia Teknolojia ya akili bandia ***(Artificial Intelligence)*** kusaidia Mamlaka ya Serikali Mtandao kujibu maswali ya mara kwa mara kuhusiana na utendaji kazi wa Mamlaka ***(ChatAI)***;

Ubunifu wa ndani wa mtandao wa 'Blockchain' unaohimiza matumizi ya mtandao wa 'Blockchain' kutengenza mifumo mbalimbali ***(Alphachain Blockchain Network),*** ubunifu wa mtandao unaotokana na Teknolojia ya ***'Blockchain'*** yenye malengo ya kuongeza ulinzi kwenye matumizi na utumaji wa nyaraka mbalimbali ***(Sec doc)***;

Mingine ni Mfumo wa kutuma, kupokea na kufuatilia malalamiko, mapendekezo, maulizo na pongezi kwenda kwa Taasisi mbalimbali za Umma ***(e-Mrejesho)***, Mfumo wa kuratibu vikao vya bodi na kamati zake, Menejimenti na kamati zake pamoja na Madiwani ***(e-Board);***

Ubunifu wa mtandao wa kijamii ulio salama ulioundwa kwa lengo la kufanya mawasiliano kupitia simu za mkononi kwa njia ya ujumbe mfupi wa maandishi, simu za sauti pamoja na simu za video ***(Oxygen)*** na ubunifu wa Teknolojia unaofanania na ***'TeamView'*** na ***'Anydesk'*** unaoruhusu kubadilishana skrini za kompyuta kwa watu walio kwenye maeneo tofauti ya kijografia ambao pia unaruhusu utumaji na upokeaji wa majalada mbalimbali kwa njia ya kielectroni ***(RSS).***

Aidha, wananchi waliotembelea katika banda la e-GA licha ya kufurahishwa na bunifu za mifumo hiyo, pia waliishauri Mamlaka kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu mifumo hiyo na namna inavyotumika.

Maonesho ya wiki ya Ubunifu Tanzania mwaka 2023 yaliandaliwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kushirikisha na Taasisi za Elimu ya Juu, Taasisi za Utafiti na Maendeleo, Vyuo vya Ufundi, Mashirika na Taasisi za Umma, Mashirika na Taasisi binafsi za Teknolojia, Wizara mbalimbali na wabunifu walioendeleza katika programu ya MAKISATU.



# TAASISI ZA UMMA ZAHIMIZWA KUENDESHA VIKAO KWA NJIA YA MTANDAO KUPUNGUZA GHARAMA 13




Meneja Mawasiliano Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), Bi. Subira Kaswaga, amezitaka Taasisi za Umma nchini kuendesha vikao kidijitali kwa kutumia mfumo wa e-Mikutano ili kupunguza gharama za uendeshaji wa vikao.

Kaswaga alitoa rai hiyo Juni 12, Mwaka huu alipofanya mazungumzo na mwandishi wetu ofisini kwake jijini Dodoma kuhusu faida zitokanazo na mfumo wa e-Mikutano.

Alibainisha kuwa, mfumo wa e-Mikutano unawawezesha watumishi wa Taasisi za umma kufanya vikao kidijitali mahali walipo bila kulazimika kukutana mahali pamoja na hivyo kusaidia kupunguza gharama za uandaaji na uendeshaji wa vikao.

***"Mfumo huu wa e-Mikutano unazisaidia taasisi za umma kupunguza gharama za uendeshaji wa vikao, kwani watumishi hawalazimiki kusafiri na kukutana mahali pamoja ili kufanya vikao na badala yake wanaweza kufanya vikao mahali walipo", alisisitiza.***

Aliongeza kuwa, mfumo wa e-Mikutano huokoa muda ambao watumishi wangeutumia kusafiri kutoka eneo moja kwenda eneo jingine kwa ajili ya kufanya vikao na hivyo kutumia muda huo kutekeleza majukumu yao mengine hali inayopelekea kuongeza ufanisi.

"Mfumo huu pia unasaidia kupunguza au kuondoa kabisa gharama za kulipia leseni zinazohitajika ili taasisi za umma ziweze kutumia mifumo ya uendeshaji wa vikao kidijitali iliyojengwa na makampuni binafsi", alifafanua.

Alisema, Mamlaka ya Serikali Mtandao ilitengeneza Mfumo wa e-Mikutano, baada ya kuona uhitaji mkubwa wa matumizi ya TEHAMA kwenye eneo la kuratibu mikutano kwa watumishi wanaokuwa katika mazingira tofauti.

Mfumo wa e-Mikutano ni rahisi na rafiki kutumia kwani mtumishi yeyote wa umma mwenye barua pepe ya serikali (GMS), anaweza kuandaa kikao na kualika washiriki wengine, na pia mfumo unawezesha kuwasiliana kwa njia ya sauti na video, alifafanua.

Mfumo wa e-Mikutano umetengezwa na wataalamu wazawa kutoka Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) na pia ni mfumo salama kwakuwa, umetengezwa kwa kuzingatia usalama mkubwa kwa watumiaji.

# UJAZA JI NA UTENGENEZAJI WA DODOSO SASA NI KIDIJITALI

14




Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) imefanikiwa kutengeneza mfumo shirikishi wa kidijitali wenye usalama na gharama nafuu unaomuwezesha mwananchi au taasisi kutengeneza na kujaza dodoso, kupata tathmini pamoja na takwimu za dodoso kwa njia ya mtandao.

Hayo yalibainishwa na Meneja wa Kituo cha Utafiti na Ubunifu na Uendelezaji wa Serikali Mtandao (eGovRIDC) cha e-GA, Mhandisi Dkt. Jaha Mvulla Juni 06, Mwaka huu alipofanya mazungumzo na mwandishi wetu ofisini kwake Jijini Dodoma.

"Mamlaka tuliamua kutengeneza mfumo huu ili kuwepo na mfumo shirikishi na salama wa kuhifadhi takwimu zinazotokana na madodoso, kuzuia urudufu wa utengenezaji wa madodoso, pamoja na kupunguza gharama kutoka kwenye mifumo ya dodoso inayotumia leseni" alisema Dkt. Jaha.

Alifafanua kuwa, mfumo huo umegawanyika katika sehemu kuu mbili ambazo ni dodoso LITE na dodoso PRO ambapo, katika utengenezaji wa maswali na upatikanaji wa takwimu katika dodoso LITE umefanywa kuwa urahisi zaidi ili kumrahisishia mtumiaji katika kujaza au kutengeneza dodoso.

Walengwa wakuu wa mfumo huu ni Taasisi za Umma na wananchi wenye uhitaji wa kutengeneza madodoso ili waweze kupata takwimu au majibu sahihi ya dodoso husika, alisema Jaha.


"Mfumo huu una uwezo wa kuhifadhi data pia ni salama kwakuwa umejengwa na wataalamu wazalendo wa ndani na unawaruhusu watumishi kufanya uchambuzi, kuhifadhi na kupata takwimu za madodoso ya taasisi yanayotengenezwa, pia taasisi au mtu binafsi anaweza kutengeneza dodoso muda wowote na mahali popote kwa njia ya mtandao" alisema Jaha.

Aidha, mtumishi anaweza kutengeneza dodoso la taasisi na kugawa namba ya dodoso na nywila kwa wahusika tu ili waweze kujaza na pia, mfumo unaruhusu na kuziwezesha taasisi kutengeneza maswali katika fomati mbalimbali na kutumia njia ya program ya simu au Kivinjari katika kujaza dodoso.

Kwa sasa Mfumo huu unapatikana bila gharama yoyote kupitia ***https://edodoso.gov.go.tz,*** ili taasisi iweze kuunganishwa na kutumia mfumo huu, taasisi husika inapaswa kuwasiliana na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) kupitia Dawati la Msaada ***http://helpdesk.ega.go.tz/ au kwa Simu namba 0764 292 299 / 0763 292 299.***

# OXYGEN :
# PROGRAMU YA KIJAMII YA MAWASILIANO ILIYOTENGENEZWA NA VIJANA WA KITANZANIA

15




Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) imetengeneza programu ya kijamii ya mawasiliano iitwayo Oxygen inayowezesha kufanya mawasiliano kwa njia ya mazungumzo, ujumbe mfupi (SMS), sauti, video, picha pamoja na aina mbalimbali za mafaili.

Programu hii inafanya kazi kama programu nyingine za kijamii na shirikishi zikiwemo WhatsApp, Telegram na Skype, huku programu ya Oxygen ikiwa na vitu vingi vya ziada.


Meneja wa Kituo cha Utafiti na Ubunifu na Uendelezaji wa Serikali Mtandao (eGovRIDC) kutoka Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Dr. Jaha Mvulla, alisema lengo la programu hiyo ni kuwezesha na kurahisisha mawasiliano baina ya familia, marafiki na timu zinazofanya kazi pamoja.

‘Programu ya Oxygen inaweza kutumika kwa soga za faragha na umma kwa kuwawezesha watumiaji kuwasiliana kwa njia ya sauti, video, jumbe fupi (SMS), picha na mafaili ‘ alifafanua Dr. Jaha.

Alieleza kuwa, Programu hii imetengezwa kwa ajili ya kusaidia watumiaji kuwasiliana kwa njia mbalimbali kwa kuzingatia usalama wa hali ya juu wa taarifa za watumiaji (end-to-end encryption).


‘Programu hii inaweza kutumiwa na mwananchi yeyote kinachohitajika ni mtumiaji kuwa na namba ya Simu pamoja na kifaa kinachoweza kutumika kama vile Simu janja (smartphone) au kompyuta kupitia kivinjari (browser)’ Alifafanua.

Programu ya Oxygen imetengenezwa na vijana wa kitanzania kupitia Kituo cha Utafiti na Ubunifu na Uendelezaji wa Serikali Mtandao (eGovRIDC) cha e-GA na imeshauriwa wananchi kutumia programu hii ili kuendeleza bunifu za ndani.



# e-GA YAPATA HATI SAFI

16



Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) ***Dkt. Mussa Kissaka*** (Kushoto) akipokea Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (CAG) ya ukaguzi wa taarifa za Fedha kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ya Mamlaka ya Serikali Mtandao kutoka kwa mkurugenzi mkuu ***Eng. Benedict Ndomba*** ambapo Mamlaka imepata hati safi. Makabidhiano hayo yalifanyika katika Ofisi za e-GA zilizopo Jijini Dae Es Salaam wakati wa kikao cha Bodi ya Wakurugenzi wa e-GA , Mei 2023









# Bodi ya Wahariri

**Mwenyekiti :** Mhandisi Benedict B Ndomba

**Mhariri :** Subira Kaswaga

**Mhariri Msaidizi :** Rainer Budodi

**Waandishi :** Catherine Peter
Queenter Mawinda

**Msanifu wa Picha :** Edger Msamba

**Mpiga Picha :** Mussa Enock

Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma
na Utawala Bora
**e-Government Authority,**
Mji wa Serikali, Mtaa wa Mtandao,
S.L.P 2833, Dodoma
Barua pepe: info@ega.go.tz
Tovuti: www.ega.go.tz

**Kwa mawasiliano zaidi, wasiliana nasi kupitia Dawati la Huduma kwa Wateja (HelpDesk);**

**0764 292 299 / 0763 292 299**
**egov.hepdesk@ega.go.tz**

*- Karibu tujenge Serikali kidijitali -*